Australian
Human Rights
Commission
everyone, everywhere, everyday

# Kufanya malalamiko

Tume ya Haki za Binadamu ya Australia ni shirika huru ambalo linachunguza na kutatua malalamiko kuhusu ubaguzi usio halali, wa jinsia, rangi, ulemavu na umri, ubaguzi wa ILO III na uvunjaji wa haki za binadamu.

## Unaweza kulalamika kwetu kuhusu nini?

- ***Ubaguzi wa jinsia*** ni pamoja na unyanyasaji wa kingono na ubaguzi unaotegemea jinsia, nafsi ya kijinsia, hadhi ya jinsia mbili, ujauzito, hali ya ndoa au uhusiano, kunyonyesha, majukumu ya kifamilia na mwelekeo wa kijinsia.
- ***Ubaguzi wa ulemavu*** ni pamoja na ubaguzi unaotegemea ulemavu wa mwili, wa akili, wa ufahamu, wa kujifunza na wa magonjwa ya akili; magonjwa; hali ya kimatibabu; majeraha yanayohusiana na kazi; ulemavu wa zamani, wa sasa na wa siku zijazo; misaada ya ulemavu; wanyama wasaidizi na kushirikiana na mtu mwenye ulemavu.
- ***Ubaguzi wa rangi*** ni pamoja na chuki na ubaguzi wa rangi kulingana na mbari, rangi, ukoo, asili ya kitaifa au kabila na hali ya wahamiaji.
- ***Ubaguzi wa umri*** ni pamoja na ubaguzi kulingana na kuwa mdogo sana au mzee sana.
- ***Ubaguzi wa ILO III*** ni pamoja na ubaguzi katika ajira kutegemea na dini, rekodi ya uhalifu, shughuli za chama cha wafanyakazi, maoni ya kisiasa na asili ya kijamii.
- ***Haki za binadamu*** ni pamoja na vitendo vya au kwa niaba ya Jumuiya ya Madola ambayo inadaiwa kuvunja vyombo maalum vya haki za binadamu vya kimataifa, kama Agano la Kimataifa juu ya Haki za Kiraia na Siasa, Mkataba wa Haki za Mtoto na Mkataba wa Haki za watu wenye Ulemavu.

Unaweza kufanya malalamiko bila kujali mahali unapoishi nchini Australia na hagharimu chochote kufanya malalamiko. Hatua katika mchakato wa malalamiko zimeelezewa hapa chini.

## Fanya uchunguzi

- Ikiwa huna uhakika ikiwa unaweza kutoa malalamiko juu ya jambo fulani, unaweza kuwasiliana na Huduma ya Habari ya Tume ya Kitaifa kwa simu kwenye **1300 656 419** au kwa barua pepe kwa infoservice@humanrights.gov.au
- Tunaweza kukutumia fomu ya malalamiko kuanza mchakato.

- Ikiwa hatuwezi kukusaidia, tutajaribu kukuelekeza kwa mtu anayeweza.

## Toa malalamiko

- Malalamiko yanapaswa kuwa kwa maandishi. Unaweza kujaza fomu ya malalamiko na kuipeleka kwetu kwa posta au feksi au unaweza kuweka malalamiko mtandaoni kwenye tovuti yetu www.humanrights.gov.au.

- Unaweza kulalamika kwa lugha unayopendelea na tunaweza kukusaidia kuandika malalamiko yako ikiwa ni lazima.

- Hutahitaji mwanasheria ili kutoa malalamiko.

- Ikiwa hatuwezi kushughulikia malalamiko yako, tutaelezea ni kwanini.

## Uchunguzi

- Tutawasiliana na wewe kuzungumza juu ya malalamiko yako na tunaweza kukuuliza kututoa habari zaidi.

- Kwa ujumla, Tume itawasiliana na mtu au shirika unalolalamika juu yake na itawape nakala ya malalamiko yako. Tunaweza kuwaomba kutoa habari maalum na/au majibu kwa malalamiko yako. Habari iliyotolewa kwa Tume kwa kujibu malalamiko yako inaweza kuwa na habari za kibinafsi, pamoja na za siri, kuhusu wewe.

- Katika kesi zingine, tunaweza kuamua kutoendelea kushughulikia malalamiko yako. Ikiwa hii itatokea, tutaelezea ni kwa nini.

- Tunaweza kuzungumza nawe juu ya kujaribu kutatua malalamiko hayo kupitia upatanisho.

## Upatanisho

- Upatanisho unamaanisha kuwa tunajaribu kukusaidia wewe na mtu au shirika unalalamika juu yake kutafuta njia ya kutatua suala hilo.

- Upatanisho unaweza kutokea katika mkutano wa uso kwa uso unaoitwa 'mkutano wa kupatanisha' au kupitia mkutano wa simu. Katika hali nyingine, malalamiko yanaweza kutatuliwa kwa kubadilishana baruapepe na mazungumzo na mpatanishaji.

- Malalamiko yanaweza kutatuliwa kwa njia nyingi tofauti. Kwa mfano, na msamaha, badiliko ya sera au fidia.

## Kitendo kinachowezekana cha korti – ubaguzi wa jinsia, ulemavu, rangi na umri

- Tume haina nguvu ya kuamua kama ubaguzi usio halali umetokea.

- Ikiwa malalamiko yako hayatatatuliwa au yamekataliwa kwa sababu nyingine, unaweza kupeleka kesi hiyo mahakamani. Korti inaweza kuamua ikiwa ubaguzi usio halali umetokea.

- Una siku 60 kuanzia wakati Tume inamaliza malalamiko ya kutuma maombi katika Korti ya Shirikisho la Duru ya Australia au Korti ya Shirikisho la Australia.

- Tume haiwezi kupeleka kesi mahakamani kwa niaba yako au kukusaidia kuwasilisha kesi yako Mahakamani.

- Unaweza kuhitaji kuzungumza na mwanasheria au huduma ya kisheria ikiwa unataka kwenda kortini.

## Uamuzi/Ripoti – ubaguzi wa ILO III na haki za binadamu

- Ikiwa malalamiko hayajatatuliwa au kukataliwa kwa sababu nyingine, Rais wa Tume anaweza kuamua ikiwa ubaguzi wa ILO III au uvunjaji wa haki za binadamu umetokea.

- Ikiwa Rais ameridhika kwamba ubaguzi au uvunjaji wa haki za binadamu umetokea, Rais anaweza kutaarifa suala hilo kwa Mwanasheria Mkuu wa Shirikisho. Katika ripoti hiyo, Rais anaweza kupendekeza fidia kwa hasara yoyote au jeraha lolote ambalo mtu amepata. Ripoti hiyo inaweza kuwasilishwa Bungeni.

- Mifano ya maamuzi ya Rais kuhusu ubaguzi na haki za binadamu yanapatikana kwenye tovuti ya Tume kwa http://www.humanrights.gov.au/publications/reports-minister-under-ahrc-act.

## Ni wapi naweza kupata habari zaidi?

Habari za mawasiliano ya Tume ya Haki za Binadamu ya Australia ni:

**Simu**
Huduma ya Habari ya Kitaifa: 1300 656 419 au (02) 9284 9888
TTY: 1800 620 241 (bila malipo)
Feksi: (02) 9284 9611

Ikiwa unahitaji mkalimani unaweza kupigia simu kwenye **131 450** na uliza kuunganishwa na Tume ya Haki za Binadamu ya Australia.

Ikiwa wewe ni kiziwi au una shida ya kusikia unaweza kuwasiliana nasi kwa TTY kwenye 1800 620 241. Ikiwa wewe ni kiziwi au una shida ya kusikia au kusema unaweza pia kuwasiliana nasi kupitia Huduma ya Ujumbe wa Zamu wa Kitaifa (NRS) kwenye 133 677. Ukihitaji mkalimani wa Auslan, tunaweza kumpanga kwako.

Ikiwa wewe ni kipofu au una shida ya kuona, tunaweza kutoa habari kwa njia mbadala kwa ombi.

**Posta**

GPO Box 5218
Sydney NSW 2001

**Mtandaoni**
Baruapepe: infoservice@humanrights.gov.au
Tovuti: www.humanrights.gov.au

Unaweza kutoa malalamiko mtandaoni kwa kwenda http://www.humanrights.gov.au/complaints/lodging-your-complaint..

## *Ushauri wa kisheria cha jumla*

Ikiwa unafikiria kuhusu kutoa malalamiko, unaweza kutaka kupata ushauri wa kisheria. Kuna huduma za kisheria za jamii zinazoweza kutoa ushauri bure kuhusu ubaguzi na unyanyasaji.

Unawez kwasiliana na shirika la Msaada wa Kisheria (https://www.nationallegalaid.org/for-individuals/) au kituo cha kisheria cha jamii cha karibu kwako www.naclc.org.au/directory.

**Kanusho: Habari kwenye karatasi hii ya ukweli inakusudiwa tu kama mwongozo. Sio mbadala wa ushauri wa kisheria.**